

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1055, ARUSHA

Simu : (027) 2503538/ 2507928

Nukushi: (027) 2505973

Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz

Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

JULAI 06, 2020

MWANANCHI AKAMATWA KWA KUMHONGA ASKARI POLISI

TAKUKURU Mkoani Arusha, mnamo tarehe 03.07.2020 ilimkamata Raphael Kivuyo mkazi wa Kijiji cha Sanawari kilichopo Kata ya Moivo Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, kwa kosa la kushawishi na kumhonga Askari Polisi mwenye namba E6969, S/Sgt Meshack Samson wa Kituo cha Polisi Sekei – Jijini Arusha.

Mwananchi huyo alishawishi fedha kiasi cha shilingi laki mbiili na elfu hamsini (sh. 250,000/-) ili askari huyo aweze kumwachia mke wake Fortunata Raphael aliyekuwa amekamatwa kwa kosa la kujihusisha na biashara ya pombe haramu ya Moshi (Gongo).

Mtuhumiwa huyo anatarajiwa kufikishwa mahakamani leo tarehe 06.07.2020 kwa kosa la kushawishi na kutoa Rushwa ambalo ni Kinyume na Kifungu cha 15 (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Ufafanuzi wa Makosa:

TAKUKURU mkoani Arusha, ilipokea taarifa mnamo tarehe 03.07.2020 kutoka kwa S/Sgt Meshack Samson ambaye ni askari polisi wa Kituo cha Polisi Sekei, akieleza kwamba Raphael Kivuyo alikuwa anamshawishi kumhonga fedha kiasi cha shilingi laki mbiili na elfu hamsini (shilingi 250,000/-) ili amwachie mke wake Fortunata Raphael aliyekuwa amekamatwa na kuwekwa mahabusu tangu tarehe 01.07.2020 kwa kujihusisha na biashara ya pombe haramu ya Moshi.

S/Sgt Meshack anaeleza kwamba baada ya kumkamata Fortunata, mnamo tarehe 02.07.2020 alipigiwa simu na mtu aliyejitambulisha kuwa ni Raphael Kivuyo, mume wa Fortunata na kumuomba amsaidie ili mke wake asifikishwe mahakamani.

Anasema yeye alimweleza kuwa hawezi kumsaidia chochote kwani suala hilo liko rasmi kiupelelezi. Hata hivyo, Afande Meshack anasema kuwa siku hiyo hiyo majira ya saa tatu asubuhi, Raphael alifika kituo cha Polisi Sekei na kumuulizia na kufanikiwa kumpata. Anaeleza kwamba baada ya kukutana, Raphael alianza kumshawishi kumpatia shilingi laki moja na elfu hamsini (Shilingi 150,000/-) ili mke wake afutiwe shitaka linalomkabili. Anasema alimkatalia ombi hilo lakini Raphael aliendelea kumshawishi hata baada ya kuachana kwa kumpigia simu mara nyingi, lakini akawa hazipokei.

Mnamo tarehe 03.07.2020 Raphael alifika tena kituo cha polisi Sekei akiwa na mwenzake na kumweleza Afande Meshack kuwa walikuwa wamekuja na shilingi laki mbili na nusu (Shilingi 250,000/-). Anasema baada ya kuona Raphael ameng'ang'ani sana kumhonga, alitoa taarifa TAKUKURU ambao waliandaa mtego na kumkamata.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawapongeza watumishi wa umma wanaokataa kupokea rushwa ili kupindisha ukweli au kukiuka taratibu zao za kiutumishi. Hii inasaidia kuwadhibiti wananchi wanaodhani kwamba rushwa inaweza kuwasaidia kukwepa mkono wa sheria.

TAKUKURU mkoa wa Arusha inazidi kuwaomba watumishi na wananchi wote wa mkoa huu kuendelea kutoa ushirikiano ili tatizo la rushwa liweze kushughulikiwa kutoka pande zote.

TAKUKURU mkoa wa Arusha inawaonya wananchi wa mkoa wa Arusha kutowashawishi watumishi wa umma ili kukiuka taratibu au kupata haki, kwani kwa kufanya hivyo ni kosa la jinai na badala yake wafuate sheria, kanuni na taratibu ili kuepuka kujiingiza kwenye vitendo vya rushwa.

Wananchi wanapaswa kuelewa kwamba mtoaji na mpokea rushwa wote wana makosa, isipokuwa pale tu mmoja wao atakapo amua kufichua uovu huo.

Imetolewa na:

JAMES G. RUGE

Signed

KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA
